**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2018

**WILAYA YA KISARAWE**



KAULI MBIU:
ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA; WEKEZA SASA KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU

**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPITIWA NA MWENGE WA UHURU TAREHE 16.07.2018**

*Imetayarishwa na:-*
*Ofisi ya Mkuu wa Wilaya*
*S.l.p 28003*
*Kisarawe*

***Julai 2018***


**RATIBA YA MBIO ZA MWENGE MWAKA 2018 WILAYA YA KISARAWE**

| MUDA | TUKIO | UMBALI KM | MAHALI | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 12:00Asubuhi | Msafara kuelekea eneo la mapokezi | 17Km | Airport | DC,KUU, Watumishi na wageni |
| 1:00-3:30 Asubuhi | Kuwasili eneo la Mapokezi<br>• Kupokea Mwenge wa Uhuru<br>• Wimbo maalum wa Mwenge<br>• Burudani: kikundi hamasa na mdundiko | | Airport | DC & wote |
| 3:30- 4:10 Asubuhi | Msafara kuelekea chuo cha FDC | 19.8 Km | Sanze | DC &wote |
| 4:10 -4:20 Asubuhi | Msafara kuwasili na kutembelea chuo cha FDC<br>• Ujumbe wa Mwenge<br>• Utekelezaji wa utoaji mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana<br>• Maonesho wanafunzi FDC, YEE | | Sanze | Kiongozi mbio za Mwenge |
| 4:20 -4:25 Asubuhi | Msafara kuelekea Seminary | 0.5Km | Sanze | DC &wote |
| 4:25- 5:25 Asubuhi | Kuwasili eneo la chai<br>• Kupata kifungua kinywa na<br>• kutembelea uwekezaji katika elimu.<br>• Salamu za Mwenge | | Sanze | DC &wote |
| 5:25 – 7:00 Mchana | Msafara kuelekea mradi wa madarasa – Yombolukinga | 70Km | Yombolukinga | DC & wote. |
| 7:00 – 7:33 Mchana | Msafara kuwasili Yombolukinga<br>• Uzinduzi mradi wa madarasa<br>• Zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri<br>• Burudani : hamasa<br>• Gawio la michango ya mwenge | | yombolukinga | Kiongozi mbio za Mwenge. |

| MUDA | TUKIO | UMBALI KM | MAHALI | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 7:33- 7:20 Mchana | Msafara kuelekea mradi wa barabara - Titu | 18Km | Titu | DC & wote |
| 7:20- 7:35 Mchana | Msafara kuwasili Titu<br>• Kuweka jiwe la Msingi katika daraja | | Titu | Kiongozi mbio za Mwenge |
| 7:35- 8:00 Mchana | Msafara kuelekea Chole Sekondari | 10Km | Chole | DC & wote |
| 8:00- 9:00 Mchana | Msafara kuwasili chole Sekondari<br>• Burudani<br>• Kupata chakula cha Mchana | | Chole | DC & wote |
| 9:00- 9:10 Alasiri | Msafara kuelekea mradi wa Majengo kituo cha Afya - Chole | 05Km | Chole | DC & wote |
| 9:10-9:15 Alasiri | Kuwasili Chole<br>• Kutembelea majengo ya Kituo cha Afya | | Chole | Kiongozi mbio za Mwenge |
| 9:15-9:20 Alasiri | • Kuona na kupokea Taarifa za shughuli za Mapambano dhidi ya **MALARIA** | | Chole | Kiongozi mbio za Mwenge |
| 9:20-9:25 Alasiri | • Kuona na kupokea Taarifa za shughuli za mapambano dhidi ya **UKIMWI** | | Chole | Kiongozi mbio za Mwenge |
| 9:25-9:30 Alasiri | • Kuona na kupokea Taarifa za shughuli za mapambano dhidi ya **MADAWA YA KULEVYA** | | Chole | Kiongozi mbio za Mwenge |
| 9:30- 4:00 Jioni | Msafara kuelekea Maneromango sekondari | 25Km | Mango Sokoni | DC &wote |
| 4:00- 4:15 Jioni | Msafara kuwasili maneromango Sekondari<br>• Kutembelea Klabu ya rushwa–sekondari<br>• Mazoezi ya sayansi kwa vitendo (kemia) | | Mango Sokoni | Kiongozi mbio za Mwenge. |
| 4:15- 4:20 Jioni | Msafara kuelekea maneromango ofisi ya Kata | 2km | Mango sokoni | DC & wote. |

| MUDA | TUKIO | UMBALI KM | MAHALI | MUHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 4:20- 4:25 Jioni | Msafara kuwasili ofisi ya Kata<br>• Uzinduzi ofisi ya Kata | | Mango Sokoni | Kiongozi mbio za Mwenge. |
| 10:25-11:00 Jioni | Msafara kuelekea eneo la Mkesha<br>- | 33Km | Mitengwe | DC &wote |
| 11:00-12:00 Jioni | Msafara kuwasili eneo la mkesha<br>• Kukagua mabanda ya wajasiliamali,Upimaji VVU,Uthibiti wa dawa za kulevya<br>• Wimbo wa Taifa<br>• Kusoma Risala ya Utii kwa Mh Rais | | Mitengwe | Kiongozi mbio za Mbio za Mwenge |
| 12:00-2:00 Usiku | Burudani na hamasa kutoka kwa vikundi mbalimbali<br>- Burudani: wasanii | | Mitengwe | Mshereheshaji |
| 2:00-3:30 Usiku | Chakula wote<br>• Utowaji wa zawadi | | Mitengwe | Kamati ya chakula |
| 3:30-11:00 Asubuhi | Mkesha | | Mitengwe | Mratibu |
| 11:00-12:00Asubuhi | Chai na usafi | | Mitengwe | Wote |
| 12:00-12:30Asubuhi | Kupokea Taarifa ya upimaji VVU | | Mitengwe | DC |
| 12:30-2:00 Asubuhi | Msafara kuelekea Kibaha Dc **(Soga)** | 22Km | Mitengwe | Kiongozi mbio za Mbio za Mwenge |
| 2:00-3:00 Asubuhi | Makabidhiano | | Soga | DC |
| 3:00- 5:00 Asubuhi | Msafara Kurejea Kisarawe | 72Km | kisarawe | DC |

## RAMANI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU WILAYA YA KISARAWE 2018



**GHARAMA ZA MIRADI NA WACHANGIAJI**

**MCHANGANUO WA GHARAMA NA WACHANGIAJI UNAOONESHA NGUVU ZA WANANCHI, HALMASHAURI YA WILAYA NA SERIKALI KUU**

| NA | AINA YA MRADI | MAHALI | JAMII | HALMASHAURI | SERIKALI KUU | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Kutembelea Uwekezaji wa elimu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi FDC | Sanze | 0.00 | 1,600,000.00 | 110,000,000.00 | 111,600,000.00 |
| 02. | Uwekezaji wa elimu Kisarawe Junior Seminari | Sanze | 0.00 | 0.00 | 5,185,850,651.00 | 5,185,850,651.00 |
| 03. | Ujenzi wa madarasa 3, ofisi na vyoo matundu 2 na Ukarabati wa Vyoo Matundu 9 shule ya msingi Yombo lukinga | Yombolukinga | 4,000,000.00 | 18,500,000.00 | 66,600,000.00 | 89,100,000.00 |
| 04. | Ujenzi wa daraja kwenye barabara ya Chole-Kihare-Vikumburu | Titu | 0.00 | 0.00 | 421,558,894.00 | 421,558,894.00 |
| 05. | Ujenzi wa nyumba ya mganga, wodi ya wazazi, wodi ya upasuaji na maabara kituo cha afya Chole | Chole | 0.00 | 0.00 | 400,000,000.00 | 400,000,000.00 |
| 06 | Kutembelea Klabu ya wapinga Rushwa maneromango Sekondari | Maneromango | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 07. | Ujenzi wa ofisi ya Kata Maneromango | Maneromango | 4,844,000.00 | 12,460,000.00 | 8,696,000.00 | 26,000,000.00 |
| | | **JUMLA KUU** | **8,844,000.00** | **32,560,000.00** | **6,192,705,545.00** | **6,234,109,545.00** |

**TAARIFA YA UWEKEZAJI WA ELIMU CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI KISARAWE KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16.07.2018**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, ndugu Charles Francis Kabeho**
Chuo cha Maendeleo ya wananchi Kisarawe kimerithi Majengo ya shule ya kati ya wasichana (Middle School) ikimilikiwa na Kanisa la Kilutherani (KKKT) kuanzia mwaka 1975 baada ya Kanisa la Kilutheri kukabidhi kwa Serikali majengo hayo mwaka 1970. Kwa wakati huo vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilikuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Taifa, mwaka 1990 vyuo vilihamishiwa kwenda Wizara ya Serikali za mitaa na masoko.
Baada ya muda mfupi tena vikamilikishwa Wizara ya Jamii Wanawake na Watoto na kisha Wizara ya Afya kwa sasa Vyuo vipo chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

**MAHALI CHUO KILIPO**

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kisarawe kipo Mkoa wa Pwani Wilaya ya Kisarawe, Tarafa ya Sungwi, Kata ya Kazimzumbwi, Kitongoji cha Sanze, ambacho kipo katika mlima wa matumaini kilometa 32 kutoka Jijini Dar es salaam na kilometa 2 kutoka Kisarawe Mjini.

**MIPANGO YA CHUO**

1. Kutoa mafunzo yenye kuongeza maarifa, stadi na mbinu mbalimbali za kutanzua matatizo halisi ya Wananchi ili wajiletee maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo
2. Mwisho wa Mafunzo wanachuo/washiriki wawe na uwezo wa kushirikiana na Asasi nyingine za Serikali, Madhehebu ya dini mbalimbali na mashirika yasiyo ya kiserikali na Wananchi kubuni na kutekeleza program na miradi madhubuti ya kutokomeza janga la UKIMWI na umaskini na kupiga vita rushwa.
3. Mwisho wa mafunzo Mwanachuo mshiriki awe na uwezo wa Kubuni na kuendesha Programu mbalimbali zitakazoinua kiwango cha fikra, maarifa na stadi za wananchi kuhusu mazingira yao na ulimwengu kwa ujumla
4. Mwanachuo/Mshiriki awe na uwezo wa kuendesha program mbalimbali za hifadhi ya mazingira kwa wananchi zinazohusu matumizi bora ya Ardhi kwa kuzingatia kanuni za kilimo na ufugaji, miti na maua, utunzaji wa vyanzo vya maji.
5. Kuanzisha mradi wa kuchakata Mhogo na kutengeneza unga kwa kuwa mashine zipo tayari. Pia mradi huu utatumika kama sehemu ya mafunzo kwa wanachuo hasa somo la ujasiriamali.
6. Kuongeza kozi zingine ambazo bado hatujafanikisha kuwa nazo kama kozi ya useremela, na kilimo.

**Ndugu Mgeni Rasmi**, karibu utembelee baadhi ya fani ulizonazo hapa Chuoni kwetu

**MAFUNZO**

Chuo kinatoa Mafunzo katika fani zifuatazo

1. Ufundi Uashi
2. Umeme wa Majumbani
3. Upishi
4. Ushonaji
5. Umakanika
6. Umeme wa magari na
7. Uchomeleaji

Kutokana na mahitaji ya jamii tunao wanachuo ambao tumewadahili na kuwasajili kufanya Mitihani ya VETA kulingana na uchaguzi wa fani walizopendelea kusoma hivyo wanasoma kwa kufuata mitaala ya VETA.

**UDAHILI**

**Ndugu Mgeni Rasmi**. Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2018, Katika kipindi cha mwaka 2016-2017/18 Chuo kimeweza kupokea kutoka Serikali kuu jumla ya Shilingi 110,000,000.00 ikiwa shilingi 48,000,000.00 fedha ya chakula, shilingi 7,000,000.00 fedha ya ujenzi wa vyoo, Shilingi 35,000,000.00 fedha za ukarabati na shilingi 20,000,000.00 kwaajili ya uimarishaji wa kozi mbalimbali zinazotolewa hapa chuoni. Chuo kimepokea jumla ya shilingi 1,600,000.00 fedha kutoka Halmashauri kwa ajili ya ukarabati wa mabweni.

**Ndugu Mgeni Rasmi**, Kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru Kitaifa 2018 katika kuongeza fursa ya Elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi tunaunga kauli mbiu ya Mhe. Rais wetu Mpendwa Mhe. John Pombe Joseph Magufuli ya Tanzania ya Viwanda. Chuo tulitoa nafasi 5 za wanachuo kusoma bure bila malipo yoyote kwa wasichana waliopata mimba za utotoni na wakina mama wasiojiweza kwa Kata Jirani na Chuo katika Halmashauri yetu hata hivyo tunaendelea na kutoa nafasi hizi kwa Kata zingine zaidi.

**WATUMISHI**

Chuo kina Jumla ya Watumishi 24 chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na mmoja ni Mtumishi wa Kujitolea 14 ni Wanaume na 11 ni Wanawake.

**CHANGAMOTO**

Ndugu Mgeni Rasmi Kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018. Chuo kina Kabiliwa na Changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na

1. Chuo kutokuwa na Hati miliki ya eneo
2. Uhaba wa Maji
3. Kutokuwa na vifaa na zana za kisasa za kujifunzia na kufundishia
4. Watumishi kutolipwa stahiki zao kwa wakati ikiwa ni pesa za Uhamisho na Likizo
5. Ukosefu wa Karakana za Kisasa kwa ajili ya Mafunzo ya Vitendo

**MAFANIKIO**

Baadhi ya Mafanikio na utekelezaji ni kama ifuatavyo.

Wahitimu wengi wa Chuo chetu wamejiajiri kwa Kazi za Ufundi waliopata hapa Chuoni na wengine wameajiriwa katika taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi hivyo wanashiriki katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

**“MWENGE OYEEEEEEEEEEEEE”**

**TAARIFA YA UWEKEZAJI WA ELIMU "KISARAWE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY" KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16.07.2018**

Ndugu Mgeni Rasmi, Mhe. Charles Kabeho (Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa)
Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe,
Watendaji Wakuu wa Serikali na Taasisi za vyombo vya ulinzi naUsalama,
Viongozi wa vyama, Madiwani na Watendaji Kata wote,
Viongozi mbalimbali wa Dini mliojumuika nasi hapa,
Wageni Waalikwa na
Wananchi wote mliohudhuria sherehe hizi za Mwenge katika kituo chetu, mabibi na mabwana
Bwana Yesu Kristo asifiwe, Asalaam aleikum, Tumsifu Yesu Kristu!

**UTANGULIZI**

Kwa niaba ya Baba Askofu Dr Alex Malasusa mkuu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani; tunamshukuru Mungu aliyetupa neema ya kuwepo leo na kushiriki katika tukio hili mhimu la kitaifa. Kwa niaba ya uongozi wa KKKT- Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Bodi ya shule na Menejimenti ya "Kisarawe Lutheran Junior Seminary" napenda kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa serikali ya Mkoa wa Pwani na wilaya yetu ya Kisarawe kwa kutambua mchango wa KKKT-DMP katika utoaji wa Elimu katika nchi yetu.

Mh Mgeni rasmi, kwetu sisi imekuwa ni faraja kubwa kuwa miongoni mwa miradi inayopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu wa 2018. Tunashukuru sana na kwa heshima, kwa niaba ya Baba Askofu, naomba kuwakaribisha rasmi nyote katika kituo hiki cha Kanisa.

**1.1 HISTORIA FUPI YA SHULE**.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, shule hii ilianzishwa rasmi mwaka 1992 ikiwa na wanafunzi 40 (wasichana 20 na wavulana 20). Shule ina eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 496,125 lililopo katika kitongoji cha Sanze katika Halmashauri ya Kisarawe Mkoa wa Pwani. Shule ni ya bweni (wavulana na wasichana) ina kidato cha kwanza hadi kidato cha sita na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 600. Shule hii inamilikiwa na KKKT-Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Kwa sasa shule ina jumla ya wanafunzi 357 (Wasichana 180 na Wavulana 177); ina watumishi 41, Walimu 26 na Wafanyakazi wasio Walimu 15.

**2.0 GHARAMA ZA UJENZI WA SHULE**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, Shule hii imejengwa kwa nguvu za washarika wa KKKT-Dayosisi ya Mashariki na Pwani. Pia, kwa misaada mbalimbali toka kwa wadau wa Elimu wa ndani na nje ya nchi. Shule ina vyumba vya madarasa 10, majengo mawili ya utawala, Majengo 11 ya mabweni (matano ya wasichana na 6 ya wavulana), Jengo kwa ajili ya kulia chakula lenye jiko linalotumia mfumo wa gesi ya kupikia, Jengo la Maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi, na Jengo kwa ajili ya matibabu ya huduma ya kwanza.

Mhe Mgeni rasmi, shule ina nyumba 6 kwa matumizi ya watumishi; tuna "Generator" kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la umeme wakati wa masomo, pia, kisima cha maji. Aidha, shule ina mfumo wa kuvuna maji ya mvua na kwa ajili ya maji ya kunywa shule ina mashine maalum ya umeme kwa ajili kuchemsha na kuchuja maji ya kunywa. Thamani ya mradi huu ni shilingi za kitanzania 5,185,850,651.0

## 3.0 MAFANIKIO YA SHULE

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Lengo kuu la kuanzishwa kwa shule hii kuandaa watumishi wa Kanisa na Taifa kwa kutoa elimu katika misingi ya Kiroho, na Maadili ya Kikristo "School mission: To prepare students serve both the church and the nation" Katika mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne, shule imekuwa na wastani wa 60% ya wanafunzi wake kuwa na sifa ya kujiunga na kidato cha tano. Katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Sita shule imekuwa na wastani wa 97% ya wanafunzi kuwa na sifa ya kujiunga na vyuo vikuu na vyuo vya Elimu ya juu. Aidha, shule imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuandaa watumishi wanaotumika maeneo mbalimbali ndani ya kanisa, taifa na wengine nje ya nchi (ambao ni walihitimu katika shule yetu).

Shule ina utaratibu wa kila muhula kuendesha semina mbalimbali ili kuwawezesha wanafunzi kujitambua, kujikinga na magonjwa ya kuambukiza, kujiepusha na vishawishi, Athari za madawa ya kulevya, athari za utandawazi na kupambana na rushwa kwa kutumia wawezeshaji kutoka ndani na nje ya shule. Elimu bora ya Kiroho, Maadili na Malezi itolewayo katika shule hii inawaandaa wanafunzi wanapohitimu kulitumikia Taifa wakiwa raia wema.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, Licha ya Watanzania kunufaika na shule hii kupitia wahitimu mbalimbali. Shule imetoa ajira kwa watanzania 41 na kati ya ajira hizo wafanyakazi saba 7 ni wakazi wa maeneo yanayoizunguka shule. Hata hivyo, yako baadhi ya maeneo ya shule ambayo Dayosisi ya Mashariki na Pwani kwa utaratibu na makubaliano maalumu imeruhusu wananchi wa maeneo haya kutumia kwa kilimo cha mazao ya muda mfupi.

Shule imeweza kuwaunganisha wakuu wa shule za Msingi nne za Halmashuri ya Kisarawe na shirika lisilokuwa la Kiserikali la UPENDO na hivyo shirika hilo kugawa magodoro ya kulalia ya siyopungua 2,000 na vifaa vya elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi Sanze, Chanzige, Kibasila na Visegese.

Mh mgeni rasmi, hata hivyo uwepo wa shule hii katika eneo hili umewanufaisha wakazi wa eneo hili kwa fulsa ya kuuza vyakula kwa wanajumuiya ya seminary.

## 5.0 CHANGAMOTO.

Mheshimiwa mgeni rasmi, pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu, shule ina changamoto kadhaa kama zifuatavyo:-

- Upatikanaji wa wanafunzi wenye sifa stahiki kukidhi uwezo wa shule wa wanafunzi 600.
- Ulipaji wa ada kwa wakati na ukamilifu hii ni kutokana na uwezo au vitapato vya wazazi.
- Baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya shule kwa shughuli mbalimbli bila kibali cha shule hivyo, kuleta migogoro na Kanisa isiyo ya lazima.

## 6.0 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO.

- Kuendelea na program maalum ya mafunzo rekebishi kwa wanafunzi ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi ili kuitangaza shule kutokana na ubora wa matokeo na hivyo kuongeza idadi ya wanafunzi.
- Kuanzisha miradi mbalimbali ya kujitegemea ili kuongeza kipato kwa shule na kwa sasa miradi ya bustani na duka imekwisha anzishwa.
- Kuendelea kushirikiana na serikali ya Kijiji na Wilaya kutatua changamoto za uvamizi wa aridhi ya eneo la shule.

**7.0 HITIMISHO.**

Tunamshukuru Mungu kwa hapa tulipofika; pia tunawashukuru wadau mbalimbali wa shule walioisaidia shule kufikia mafanikio haya. Tunawaomba wasichoke kutuunga mkono tunapoendelea kukabiliana na changamoto zilizo mbele yetu.

Tunaushukuru sana uongozi wa Mkoa na Wilaya yetu ya Kisarawe kwa kuona vema ratiba ya Mwenge mwaka huu ufikie katika shule yetu ya Seminary Kisarawe ikiwakilisha sekta binafsi katika utoaji wa elimu katika Wilaya yetu.

Kwa niaba ya uongozi wa Kanisa Dayosisi ya Mashariki na Pwani; tunakutakia afya njema kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa pamoja na timu yako nzima kwa majukumu mliyonayo Kitaifa. Tunawatakia baraka za Mungu wote mliojumuika nasi hapa Seminary katika hukio hili la kihistoria katika shule yetu.

Naomba kuwasilisha!

**MWENGE OYEEEEEEEEEEEEE**

**TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA MADARASA 3, OFISI NA VYOO SHULE YA MSINGI YOMBO LUKINGA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16.07.2018**

**UTANGULIZI**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndugu Charles Francis Kabeho**
Sisi wananchi wa Kata ya Chole Kijiji cha Yombolukinga tunayo furaha kubwa kukukaribisha wewe na msafara wako kijijini kwetu kwa ajili ya kutuzindulia mradi wa ujenzi wa madarasa matatu na ofisi ya Walimu.

Mradi huu wa ujenzi wa madarasa na ofisi ulianza kutekelezwa tarehe 10/03/2018. Kutokana na changamoto ya uchakavu wa madarasa ya awali wananchi wa Yombo Lukinga walianza kujenga madarasa mawili kwa jitihada zao wenyewe na baadae serikali ikaleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa haya matatu ambayo tanaomba leo utuzindulie.

**Lengo la mradi**

Lengo la ujenzi wa madarasa na ofisi ya Walimu ni kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kuinua taaluma

**Faida ya mradi**

Faida ya mradi huu ni kuwa na mazingira bora ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi pamoja na mazingira mazuri ya kufanya kazi walimu.

**GHARAMA ZA MRADI;**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa mwaka 2018,**

Mradi huu umejumuisha ujenzi wa madarasa haya matatu,ofisi, vyoo vya walimu matundu mawili na ukarabati wa vyoo matundu 10

Gharama za mradi huu zimetokana na fedha kutoka serikali kuu kiasi cha shilingi 66,600,000.00 nguvu za wananchi shilingi 4,000,000.00 Pia Halimashauri imechangia kiasi cha shilingi 12,000,000.00 ambazo zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa madarasa mawili na ofisi ya walimu yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na shilingi 6,500,000.00 kwa ajili ya kuweka marumaru kwenye madarasa 3 na ofisi kwenye mradi wa P4R.

Kiasi kilichotumika mpaka sasa ni shilingi 65,675,930.00 kwa ujenzi wa madarasa 3 na utengenezaji wa madawati 75, ofisi ya mwalimu, ujenzi wa choo cha walimu matundu 2 na ukarabati wa matundu 10 ya vyoo (Matundu 7 ya wanafunzi wa kawaida (wasio na ulemavu), matundu 2 ya vyoo kwa ajili ya wanafunzi walemavu na chumba kimoja kwa ajili ya Wanafunzi Wasichana)

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**
Kwa heshima na tahadhima tunakuomba sasa utuzindulie mradi wetu wa ujenzi wa madarasa matatu na ofisi, na kukagua ujenzi wa madarasa 2 yanayojengwa kwa nguvu za wananchi.

**“MWENGE OYEEEEEEEEEEEEE”**

**NI SISI WANANCHI WA KIJIJI CHA YOMBO LUKINGA**

## TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA DARAJA KWENYE BARABARA YA CHOLE-KIHARE-VIKUMBURU KWA KIONGOZI WA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16.07.2018

### UTANGULIZI

**Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2018, Charles Francis Kabeho**, Kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe tunayo furaha kubwa sana kukukaribisha wewe na msafara wako.

Ujenzi wa daraja hili ulianza mwezi Februari, 2018. Hadi sasa kazi ipo kwenye hatua ya umaliziaji kwani ujenzi wa daraja na makalvati kwenye maingilio ya daraja umekamilika. Kwa sasa kazi zinazoendelea ili kukamilisha daraja hili ni Ujenzi wa kingo za mto (gabion boxes), urekebishaji wa mto (river training), Kujenga barabara ya kuingia na kutokea darajani mita 660 na kujenga kingo za daraja (guide rails) .Kukamilika kwa daraja hili kutasaidia kuimarisha shughuli za usafirishaji wa abiria na shughuli za ukuzaji wa uchumi wa Wananchi kwa maeneo ya Chole, Kihare, Kisangire, Koresa na Vikumburu kwa kipindi chote cha mwaka.

### GHARAMA ZA MRADI

**Ndugu, Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2018**, mradi huu unagharimu jumla ya shilingi **421,558,894.00**, Mradi huu upo ndani ya mkataba wa shilingi **527,891,095.30** ambapo pia mkataba huu unajumuisha ujenzi wa daraja dogo linalogharimu jumla ya shilingi **69,502,590,** kwenye barabara hii,aidha mkataba huu pia una fedha ya tahadhari kiasi cha shlingi **36,829,611.30** Fedha za mradi huu zimetolewa na Serikali kuu zikiwa ni ufadhili wa the government of the united kingdom of great Britain and Northen Ireland ya Department for development for International development (**DFID).**Mpaka kufikia hatua hii Mkandarasi wa mradi huu ameshalipwa jumla ya shilingi **256,918,154.76 (daraja shilingi 227,989,649.76 na daraja dogo shilling 28,928,505.00)**. Gharama zote hapo juu zinajumuisha kodi ya serikali (VAT). Aidha mkataba huu unamsamaha wa Kodi hivyo mpaka sasa mkandarasi amelipwa jumla ya fedha isiyo na VAT jumla ya shilingi **217,727,249.80 (daraja hili shilingi 193,211,567.60 na daraja dogo shilling 24,515,682.20).**Gharama ya kodi iliyosamehewa na serikali kwenye malipo hayo ni shilingi **39,190,904.96** ambayo ni mchango wa serikali kwenye mradi huu mpaka kufikia hatua hii ya malipo.

### FAIDA ZA MRADI

**Ndugu, Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2018**, mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kuwa na faida zifuatazo:-

- Kurahisisha usafirishaji wa abiria kwa wanavijiji vya Titu, Kihare,Kihare na Kisangire Koresa mpaka Vikumburu. Wananchi hawa watakuwa na uhakika wa usafiri kwa kipindi chote cha majira ya mwaka.
- Kurahisisha usafrishaji wa mazao kwa wakulima wa vijiji vya Kihare, Kisangire na Koresa.
- Wananchi wa Kihare, Kisangire na Koresa kuwa na Uhakika wa kufika Kituo cha Afya Chole kwa huduma zaidi za matibabu.
- Wananchi wa Vijiji vya Kihare, Kisangire na Koresa kuweza kuhudumiwa na viongozi ngazi mbalimbali kwa vipindi vyote vya majira ya mwaka.

**Ndugu, Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2018,**

Kwa heshima na taadhima tunaomba utuwekee jiwe la Msingi daraja letu lenye urefu wa mita 19.35M Aidha tunakutakia wewe na msafara wako safari njema.

**MWENGE OYEEEEEEEEEE!!!!!!!**

**TAARIFA YA UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU YA AFYA KATIKA KITUO CHA AFYA CHOLE KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16.07.2018**

**UTANGULIZI;**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, ndugu Charles Francis Kabeho,**

Sisi Wananchi wa Kijiji cha Chole tunayo furaha kubwa kukukaribisha wewe na msafara wako. Mradi wa uboreshaji wa miundo mbinu ya afya unajumuisha ujenzi wa nyumba ya Mganga,Wodi ya wazazi,jengo la a upasuaji na maabara. Mradi huu ulianza tarehe 12/02/2018. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kituo cha afya kutoa huduma kwa Wananchi hivyo kuboresha huduma za Afya hasa akina mama na Watoto.

**Lengo la mradi**

Lengo la mradi ni kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga.

**Faida ya Mradi**

Faida ya mradi huu ni kupunguza umbali wa kupata huduma ya upasuaji, upatikanaji wa huduma bora na wataalam karibu na wananchi, kupunguza gharama za rufaa kwa wagonjwa, kumpunguzia mwananchi gharama za kufuata huduma kwa mfano kwenye Hospitali ya Wilaya au Muhimbili kwa umbali wa zaidi ya kilometa 100.

**GHARAMA ZA MRADI;**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru,**

Ujenzi huu utagharimu kiasi cha Shilingi 400,000,000.00 Hadi kufikia mwezi Julai kiasi cha shilingi 335,447,100.00 kimetumika. Mchanganuo wa fedha zilizotumika hizo ni kama ifuatavyo;

| MRADI | GHARAMA | KIASI KILICHOTUMIKA |
|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba ya mganga | 60,529,800.00 | 55,820,674.00 |
| Ujenzi wa wodi ya wazazi | 130,319,745.00 | 100,787,085.00 |
| Ujenzi wa wodi ya upasuaji | 118,708,455.00 | 92,678,422.00 |
| Ujenzi wa maabara | 90,442,000.00 | 86,160,919.00 |
| **JUMLA** | **400,000,000.00** | **335,447,100.00** |

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;**

Wananchi wa Kijiji cha Chole tunatoa shkrani za dhati kwa Serikali yetu ya awamu ya Tano kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwa kufanikisha ujenzi wa Nyumba ya Mganga,wodi ya wazazi,wodi ya upasuaji na maabara. Pia tunashukuru kwa kutupa heshima kijiji chetu cha Chole kufikiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru pamoja na ujumbe wake kwa mwa 2018.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**

Kwa heshima na tahadhima tunakuomba sasa utembelee na kukagua mradi wetu wa ujenzi wa nyumba ya Mganga,wodi ya wazazi,wodi ya upasuaji na maabara.

**“MWENGE OYEEEEEEEEEEEEE”**

**NI SISI WANANCHI WA CHOLE**

**TAARIFA YA KLABU YA WAPINGA RUSHWA SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16/07/2018**

**Ndugu Kiongozi**

Tulioko mbele yako ni wananchama wa klabu ya wapinga rushwa katika Shule ya Sekondari Maneromango. Klabu yetu ina jumla ya wanachama 35 wasichana 20 wavulana 15 Klabu ya Wapinga rushwa sekondari ya Maneromango ilianzishwa mwaka 2012 na kuzinduliwa rasmi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa Capten Honest Erenest Mwanossa tarehe 1/07/2012 .

**Ndugu Kiongozi**

Klabu hii ya wapinga rushwa ilianzishwa hapa shuleni kwa lengo la kutujenga sisi wanafunzi kimaadili na kushiriki mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa elimu ya rushwa kwa vijana wenzetu na jamii inayotuzunguka kwa kutumia njia mbalimbali kama maigizo, ngojera, nyimbo na kuandaa kazi za sanaa kama vibonzo ambazo zina ujumbe unaoonyesha madhara Rushwa na jinsi ya kuiepuka.

**Ndugu Kiongozi**

Jukumu la kupambana na Rushwa si la TAKUKURU wala Serikali peke yake bali ni la kila Mwananchi. Hivyo ni wajibu wetu sote kushiriki kikamilifu katika mapambano haya kwani pamoja tutashinda kama ujumbe wa mwenge mwaka 2018 unavyoeleza “ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA WEKEZA SASA KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU”. Pia kauli mbiu dhidi ya Rushwa inayosema “KATAA RUSHWA –JENGA TANZANIA”.

Hivyo, sisi wananchama wa klabu ya wapinga rushwa shule ya Sekondari Manerumango tunashirikiana na TAKUKURU Katika kutoa elimu kwa vijana na jamii yetu ili waweze kushiriki katika mapambo dhidi ya rushwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Ndugu Kiongozi**

Kwa heshima na taadhima tunaomba wewe na hadhara yetu msikilize ujumbe tuliouandaa katika kuhamasisha mapambano dhidi ya Rushwa.

# Mwenge oyeeeeeeeeee!

**TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA OFISI YA KATA MANEROMANGO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 16.07.2018**

**UTANGULIZI;**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, ndugu Charles Francis Kabeho,**

Sisi Wananchi wa Kijiji cha Maneromango tunayo furaha kubwa kukukaribisha wewe na msafara wako katika kata ya Maneromango.

Ujenzi wa ofisi hii ya Kata ya Maneromango ulianza Disemba mwaka 2016 kwa nguvu za wananchi na baadae kupata usaidizi wa rasilimali fedha kutoka serikalini.

Jengo hili la ofisi ya kata lina vyumba 4 na ukumbi 1 wa mikutano, hatua hii imefikiwa ili kuondoa changamoto ya ukosefu wa ofisi ya Afisa mtendaji kata na Wataalam ngazi ya kata.

**LENGO LA MRADI**

Lengo la mradi huu ni kuboresha utoaji wa huduma bora kwa Wananchi na kuboresha utendaji wa Maafisa ngazi ya Kata kwa kufanya kazi katika mazingira mazuri na ufanisi.

**FAIDA ZA MRADI**

Faida ya Mradi huu ni kuimarisha utawala bora, uhifadhi wa kumbukumbu pamoja na kutoa huduma kwa ukaribu kwa wananchi.

**GHARAMA ZA MRADI;**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge,**

Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Kata Maneromango umekamilika na Fedha zilizotumika mpaka sasa ni shilingi 26,000,000.00 kati ya hizo shilingi 12,460,000.00 ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri, shilingi 8,696,000.00 fedha za ruzuku ya Maendeleo kutoka serikali kuu na shilingi 4,000,000.00 ni nguvu za wananchi wa Maneromango.

**HITIMISHO;**

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;** Wananchi wa kata ya Maneromango tunatoa pongezi kwa Serikali yetu ya Tanzania ya awamu ya Tano kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwa kufanikisha ujenzi wa ofisi ya Kata Maneromango. Pia tunashukuru kwa kutupa heshima kijiji chetu cha Maneromango kufikiwa na mbio za Mwenge wa Uhuru

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,**
Kwa heshima na tahadhima tunakuomba sasa utuzindulie mradi wetu wa ofisi ya Kata ya Maneromango.

**“MWENGE OYEEEEEEEEEEEEE”**

**NI SISI WANANCHI WA MANEROMANGO**